USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI




# DEMOKRASIA, HAKI ZA BINADAMU, NA UTAWALA BORA (DRG)

## TANZANIA

Serikali ya Tanzania imedhamiria, kwa watu wake na kwa jamii ya kimataifa, kuboresha utawala bora na wa kidemokrasia. Ingawa Tanzania bado iko juu ukilinganisha na nchi jirani kwa suala la uwazi, uwajibikaji, na haki za kiraia, kushuka kwa kasi kwa demokrasia katika miaka ya hivi karibuni kunaashiria wasiwasi. USAID inasaidia katika kuboresha hayo kwa kutekeleza miradi ambayo imejengwa siku za nyuma yenye kutoa majibu ya kukabiliana na kushuka kwa nafasi za kiraia na kisiasa, kukuza uhuru wa kujieleza, kuboresha utetezi na uwezo wa mawasiliano wa taasisi za kiraia , mashirika ya ndani, kukuza mifumo ya uwazi na uwajibikaji isiyo na rushwa, na kuimarisha haki za binadamu katika jamii, hasa kwa wale walio hatarini.

Miradi hii ina lengo la kufanikisha madhumuni manne: 1) kuboresha uwezo wa vyombo vya habari na asasi za kiraia (AZAKI) kutoa habari sahihi na zilizo na usawa; 2) kuimarisha uwezo wa washirika wa AZAKI katika maeneo yaliyolengwa; 3) kuboresha majukwaa ya mazungumzo ambayo yanakuza ushiriki wa raia; na 4) Kuboresha ushiriki wa raia na usimamimiaji katika chaguzi na michakato ya kisiasa. Kwa kuongezea,

## MAELEZO YA DRG

### KIWANGO CHA UFADHILI

- Dola za Marekani Milioni 7.5 kwa Mwaka wa Fedha 2019
- Dola za Marekani Milioni 2.5 kwa Mwaka wa Fedha 2020

### WASHIRIKI WAKUU

- Freedom House
- UN Women
- Pact
- The Consortium for Elections and Political Process Strengthening (CEPPS)
- Internews
- FHI 360

### MAENEO

Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kigoma, Manyara, Morogoro, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Njombe, Tanga, na Zanzibar, na pia msaada kwa michakato ya kisiasa katika ngazi ya kitaifa.

### MAWASILIANO

Theodore Glenn
tglenn@usaid.gov

#### KWA MAWASILIANO ZAIDI

Tovuti: www.usaid.gov/tanzania
Facebook: USAIDTanzania
Twitter: @USAIDTanzania

miradi ya USAID inasaidia kukuza uhamasishaji wa kanuni za maadili na inalenga ushiriki mkubwa wa wanawake na vijana katika michakato ya kisiasa.
Kwa pamoja, juhudi hizi zinahimiza ushiriki wa raia huku zikiongeza uhamasishaji kwa umma kuhusu majukumu, na hatua za serikali. Pia miradi hii huendeleza ushirika na juhudi za USAID kwa kila Sekta kulingana na ustadi kamili na rasilimali, malengo na mtazamo wa kijiografia ili kuongeza matokeo. Njia hii iliyojumuishwa inaimarishwa zaidi na kushirikiana kwa sekta ndogo ili kuboresha usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake na vijana.

## CHANGAMOTO

Kuboresha utawala bora nchini Tanzania ni ngumu kutokana na kuongezeka nguvu kwa mhimili wa serikali, nafasi za kisiasa kuwa adimu, ukiukaji wa haki za binadamu, ukosefu wa ushindani wa kisiasa, jumuiya ya kiraia inayoendelea kukua, uwezo mdogo wa serikali, uwajibikaji mdogo wa umma, na vizuizi vya upatikanaji wa habari. Wanawake na vijana wana shida sana katika maeneo haya. Changamoto ni pamoja na:

- Kuminya demokrasia inayotokana na mifumo isiyo halali ya kisheria, na matumizi mabaya ya mamlaka ya serikali; zinazoathiri mashirika ya kiraia, vyama vya siasa, na vyombo vya habari.

- Hatua mpya za kuzuia na kudhibiti upatikanaji wa habari, shughuli za mtandaoni, na uhuru wa kujieleza

- Kuongezeka kwa ukiukwaji wa haki, haswa kwa wanawake na idadi ya watu waliotengwa

## MATOKEO

- Wadau wa AZAKI walifanya kazi na wadau mbali mbali na walitumia njia mbali mbali za kushughulikia masuala ya haki, pamoja na uwekaji wa kimkakati, ushiriki wenye tija wa watoa maamuzi wa serikali, na ushiriki katika michakato ya mashauriano ya umma.
- AZAKI zilishiriki katika michakato ya kukagua miswada kadhaa yenye hadhi ya juu (pamoja na Sheria ya Vyama vya Siasa, Sheria ya Mashirika yasiyo ya kiserikali, Sheria ya Takwimu, na Sheria ya Kampuni) katika Bunge. Washirika wa muungano waliratibu juhudi na kutumia taaluma zao za kulinganisha. Mapendekezo yao kadhaa yameingizwa katika sheria zinazosababisha, kuboresha umoja.
- Miundo ya Uongozi na vitengo vya wanawake na vijana ndani ya vyama vyote, chama tawala na vya upinzani vimejitolea kuboresha utawala wa ndani na kufanya kazi ili kuongeza utofauti wa wagombea na watendaji wa vyama vya ndani.
- Zaidi ya waandishi wa habari 200 wa kitaifa katika mikoa tisa wamepata mafunzo ya kimsingi na ya kati kuhusu namna ya kutoa mafunzo ya kiwango cha juu ya habari za ndani, kuboresha tovuti na njia za mitandao ya kijamii,

kuongeza sauti za wanawake na vijana katika programu zao na kuboresha ubora na kuwa na usawa wa taarifa zao .

- Imeanzisha ushirikiano na Chuo cha Uandishi wa Habari na Mawasiliano, Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino cha Tanzania jijini Mwanza, na Chuo cha Uandishi wa Habari Zanzibar kuunga mkono mafunzo ya wanafunzi wa uandishi wa habari zaidi ya 600 kupitia wiki sita za mafunzo, ili kuwapa ujuzi stadi wa kazi kwa siku zijazo kwenye vyombo vya habari.
- A new partnership with the Tanzania Women's Lawyers Association will support the empowerment of women and youth; bolstering leadership in areas related to access to justice, economic participation, and community decision-making.

- Ushirikiano mpya na Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania utasaidia uwezeshaji wa wanawake na vijana; kuimarisha uongozi katika maeneo yanayohusiana na upatikanaji wa haki, ushiriki wa kiuchumi, na maamuzi ya jamii.